UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

MINISTRY OF ENERGY

ENERGY AND WATER UTILITIES REGULATORY AUTHORITY (EWURA)

# PUBLIC NOTICE

## A CALL FOR STAKEHOLDERS' VIEWS ON THE MULTI-YEAR TARIFF APPLICATION SUBMITTED BY LINDI WATER SUPPLY AND SANITATION AUTHORITY (LINDI WSSA)

On 1st April 2023, EWURA received an application from Lindi Water Supply and Sanitation Authority (Lindi WSSA) requesting approval of multiyear tariffs, charges, and fees applicable to water supply services in financial years 2023/24, 2024/25 and 2025/26. Tables 1 to 3 present tariffs, fees, and charges proposed by Lindi WSSA.

**Table 1: Current and Proposed Metered Water Tariffs (TZS/m$^3$)**

| Description | Consumption | Current tariff TZS/M$^3$ | Proposed Tariff TZS/M3 | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | M | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| Domestic | 0 – | 1,600 | 4,690 | 4,508 | 4,320 |
| | >5-9 | 1,700 | 4,983 | 4,790 | 4,591 |
| | >1 | 1,800 | 5,276 | 5,072 | 4,861 |
| Institution | | 2,100 | 6,156 | 5,917 | 5,671 |
| Commercial | | 2,200 | 6,449 | 6,199 | 5,941 |
| Industrial | | 2,200 | 6,449 | 6,199 | 5,941 |
| Kiosk | | 1,500 | 4,397 | 4,226 | 4,050 |
| Bulk Customers | | 2,300 | 6,742 | 6,481 | 6,211 |

**Table 2: Current and Proposed New Connection Fee (TZS/Connection)**

| Customer Category | Current Fees | Proposed Fees | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| Domestic | 20% of recoverable expenditures as stipulated in Section 24 of Water Supply Regulations, 2013 | 20% of recoverable expenditures as stipulated in Section 26 of Water Supply Regulations, 2019 | | |

**Table 3: Current and Proposed Reconnection Fees (TZS/Reconnection)**

| Customer Category | Current Fees | Proposed Fees | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| Domestic | 10,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 |
| Institutional | 40,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 |
| Commercial | 40,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 |
| Industrial | 40,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 |

Lindi WSSA explained that the proposed tariff adjustment will enable the utility to implement activities set out in its business plan for the period from 2023/24 to 2025/2026 in order to ensure sustainable water services delivery. Specifically, proposed tariffs and fees will enable the utility to meet operational and maintenance costs, undertake rehabilitation and replacement of dilapidated infrastructure as well as finance minor new investments including extending water services to areas without network.

This public notice is made pursuant to Section 19(4) of the EWURA Act, Cap 414, which requires the Authority to issue a notice of inquiry to collect views from stakeholders including the Government Consultative Council (GCC), Consumer Consultative Council (CCC), Lindi WSSA's customers and the general public on the reasonableness of the proposed tariffs, fees and charges. As part of the inquiry, there shall be a public hearing meeting on Thursday, 8th June 2023 at Double M Hall in Lindi Town from 10:00hrs.

Stakeholders are requested to submit written comments at any time by 15th June 2023 to EWURA Head Quarters located at EWURA House, 3 EWURA Street, Medeli West, 41104 Tambukareli, P.o.Box 2857, Dodoma, or to EWURA Eastern Zone Office, 4th Floor -Wing A, PSSSF Commercial Complex, P.O.Box 72175, Dar es Salaam or via our email address info@ewura.go.tz.

**Issued by:**
**Director General**
**EWURA**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA NISHATI

MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

## TANGAZO KWA UMMA

## MWITO WA MAONI YA WADAU KUHUSU MAOMBI YA MAREKEBISHO YA BEI YALIYOWASILISHWA NA MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA LINDI

Mnamo tarehe 1 Aprili 2023, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) ilipokea maombi ya marekebisho ya bei za huduma za majisafi fi wa mazingira kutoka Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Lindi. Majedwali Namba 1 hadi 3 yanaonesha viwango vya bei vinavyopendekezwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Lindi.

**Jedwali Na. 1: Bei za Maji za Sasa na Zinazopendekezwa (Shilingi kwa Mita ya Ujazo)**

| Kundi la Wateja | Matumizi | Bei za Sasa | Bei Zinazopendekezwa | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | $M^3$ | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| Majumbani | 0 – 5 | 1,600 | 4,690 | 4,508 | 4,320 |
| | >5-9 | 1,700 | 4,983 | 4,790 | 4,591 |
| | >10 | 1,800 | 5,276 | 5,072 | 4,861 |
| Taasisi | | 2,100 | 6,156 | 5,917 | 5,671 |
| Biashara | | 2,200 | 6,449 | 6,199 | 5,941 |
| Viwanda | | 2,200 | 6,449 | 6,199 | 5,941 |
| Magati | Lita 20 | 1,500 | 4,397 | 4,226 | 4,050 |
| Wateja Wakubwa | M3 | 2,300 | 6,742 | 6,481 | 6,211 |

**Jedwali Na. 2: Ada ya Sasa na Inayopendekezwa ya Kuunganishiwa Huduma (Shilingi kwa Maunganisho)**

| Kundi la Wateja | Ada ya Sasa | Ada Zinazopendekezwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| Majumbani | Asilimia 20% ya gharama za maunganisho kama ilivyoelekezwa katika Kanuni ya 24 ya Kanuni za Maji za Mwaka 2013 | Asilimia 20% ya gharama za maunganisho kama ilivyoelekezwa katika Kanuni ya 26 ya Kanuni za Maji za Mwaka 2019 | | |
| Taasisi | | | | |
| Biashara | | | | |
| Viwanda | | | | |

**Jedwali Na. 3: Ada za Sasa na Zinazopendekezwa za Kurejeshewa Huduma (Shlingi kwa Maunganisho)**

| Kundi la Wateja | Ada za Sasa | Proposed Fees | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| Majumbani | 10,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 |
| Taasisi | 40,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 |
| Biashara | 40,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 |
| Viwanda | 40,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 |

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Lindi imeeleza kuwa bei zilizopendekezwa zitaiwezesha mamlaka kutekeleza mpango wake wa biashara wa miaka mitatu kutoka mwaka 2023/24 hadi mwaka 2025/26 ili kuhakikisha huduma endelevu ya maji. Pia bei iliyopendekezwa itaiwezesha Mamlaka ya Maji Lindi kukidhi ongezeko la gharama za uendeshaji na matengenezo ya vipuri, kufanya ukarabati wa miundombinu chakavu ya mamlaka na kufanya uwekezaji mdogomdogo na hivyo kuhakikisha huduma endelevu ya maji katika mji wa Lindi.

Tangazo hili limetolewa kwa mujibu wa Kifungu cha 19(4) cha Sheria ya EWURA Sura ya 414, kinachoitaka EWURA kutoa tangazo la taftishi ili kukusanya maoni kutoka kwa wadai ikiwa ni pamoja na Baraza la Ushauri la Serikali (EWURA GCC), Baraza Ushauri la Watumiaji wa Huduma Zinazodhibitiwa na EWURA (EWURA CCC), Wateja wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Lindi na umma kwa ujumla kuhusu bei zinazopendekezwa. Kama sehemu ya taftishi, kutakuwa na mkutano wa kusikiliza maoni ya wadau utakaofanyika siku ya Alhamisi, tarehe 8 Juni 2023 katika Ukumbi wa Double M iliopo Lindi mjini kuanzia saa nne asubuhi.

Wadau wanaombwa kuwasilisha maoni ya maandishi kwenye ofisi za **Makao Makuu ya EWURA** zinazopatika katika **Jengo la EWURA, 3 Barabara ya EWURA, 41104 Tambukareli, S.L.P. 2857, Medeli Magharibi, Dodoma** au **Ofisi za EWURA Kanda ya Mashariki** zilizopo **Ghorofa ya Nne, Jengo la PSSSF Commercial Plaza, S.L.P. 72175, Dar es salaam** au kupitia barua pepe yetu info@ewura.go.tz wakati wowote hadi tarehe 15 Juni 2023.

**Imetolewa na:**
**Mkurugenzi Mkuu**
**EWURA**